JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 1995

MADA IMETOLEWA NA MHESHIMIWA MARGARET SITTA (MB), WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
30 JANUARI 2006

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
S. L. P. 9121
DAR ES SALAAM

1.0 UTANGULIZI

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 iliandaliwa kutokana na mapendekezo ya Tume ya Rais ya Elimu (Makwetta Commission) iliyoteuliwa mwaka 1981 ili kupendekeza mabadiliko yatakayohitajika nchini ifikapo mwaka 2000. Hali kadhalika Tume Maalum ya Taifa ya Elimu iliyoundwa mwaka 1990 ili kuangalia upya mfumo wa elimu uliokuwepo na kupendekeza mfumo wa kufaa kwa Karne ya 21. Sera hii imelenga kuoanisha, kurekebisha na kuweka sawa miundo, mipango na shughuli za elimu, kuhakikisha upatikanaji na utoaji wa fursa sawa pamoja na mbinu bora na za kufaa katika uongozi, utawala na ugharimiaji wa elimu na mafunzo nchini.

DIRA (VISION)

Kuwa na Mtanzania aliyeelimika kwa kiwango cha juu, mwenye maarifa, mahiri na aliyekomaa kiutamaduni ili aweze kukabiliana na changamoto za Kitaifa na Kimataifa katika nyanja za kisiasa, kijamii na kiuchumi ifikapo mwaka 2025.

DHIMA (MISSION)

Kutoa fursa sawa ya elimu bora kwa wote na kuhakikisha kuwepo mazingira mazuri ya kisheria na kiutendaji yenye mvuto kwa wadau wote wenye nia na uwezo wa kutoa elimu iliyo bora ili washiriki kupanua elimu hiyo katika ngazi zote pamoja na kuimarisha uendeshaji, usimamizi na miundombinu.

2.0 YALIYOMO KWENYE SERA YA ELIMU NA MAFUNZO

Sera ya Elimu na Mafunzo imefafanuliwa katika vipengele vikuu kumi (10) kama ifuatavyo:

- Madhumuni na Malengo ya Elimu na Mafunzo
- Mfumo na Muundo wa Elimu na Mafunzo
- Fursa na usawa katika utoaji wa Elimu na Mafunzo
- Uongozi na utawala katika Elimu na Mafunzo
- Mitaala, Mitihani na Utoaji Vyeti
- Elimu na Mafunzo ya Ufundi
- Elimu na Mafunzo ya Juu

- Elimu na Mafunzo Nje ya Mfumo rasmi wa Elimu, na
- Ugharimiaji wa Elimu na Mafunzo.

2.1 Madhumuni na Malengo ya Elimu na Mafunzo

Sera imeainisha madhumuni na malengo ya jumla ya elimu na mafunzo. Aidha, madhumuni na malengo ya elimu na mafunzo kwa kila ngazi ya elimu pia yameainishwa.

2.2 Mfumo na Muundo wa Elimu na Mafunzo

Mfumo wa Elimu na Mafunzo una mpangilio wa ndani kwa ndani unaoruhusu upangaji wa programu na taratibu hasa zinazohusiana na utumishi, fedha na muda ili kufanikisha malengo yaliyowekwa. Aidha, ipo mifumo midogo miwili ya Elimu na Mafunzo: Mfumo wa elimu iliyo rasmi na Mfumo wa elimu isiyo rasmi.

Elimu na Mafunzo nchini inatekelezwa na wizara zote lakini zilizo muhimu kwa elimu rasmi na ya nje ya mfumo rasmi wa elimu ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Elimu rasmi na isiyo rasmi hutolewa pia na jamii, mashirika yasiyo ya kiserikali na watu binafsi kwa uratibu wa wizara na serikali kuu.

Muundo wetu wa elimu rasmi ni wa miaka miwili ya elimu ya awali, miaka saba ya elimu ya msingi, miaka minne ya elimu ya sekondari ngazi ya kawaida, miaka miwili ya sekondari ngazi ya juu na miaka isiyopungua mitatu ya elimu ya chuo kikuu.

2.3 Fursa na Usawa katika utoaji wa Elimu na Mafunzo

Sera ya Elimu na Mafunzo inazingatia usawa katika utoaji na upatikanaji wa elimu nchini. Usawa una maana ya ulingano katika ugawaji na utoaji wa huduma za elimu kwa makundi mbalimbali ya jamii bila kujali jinsia, rangi, kabila au hadhi ya kiuchumi ya mtu au jamii kwa kiwango cha kuridhisha. Sera hii imeainisha makundi mbalimbali ya jamii na kuweka mikakati mahsusi ya kutekeleza mipango ya utoaji na upatikanaji wa elimu kwa usawa. Makundi yaliyoainishwa ni pamoja na yale yenye matatizo kutokana na mitindo yao ya kuishi na wenye ulemavu wa maumbile. Aidha, mikakati ya utoaji elimu na mafunzo kwa usawa imeainishwa yenye kujumuisha: Mfumo wa mgao maalum wa nafasi (Quota system), Utambuzi wa watoto wenye vipaji

maalum, Upatikanaji wa nyenzo stahili na za kutosha pamoja na kuboresha programu za lishe na afya katika shule na vyuo.

2.4 Uongozi na Utawala katika Elimu na Mafunzo

Uongozi wa elimu na mafunzo unafanywa na wizara kadhaa, mashirika ya umma, mashirika yasiyo ya kiserikali na watu binafsi. Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) inatambuliwa kama chombo cha kuratibu elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Vyombo vingine vimeundwa kuratibu elimu na mafunzo baada ya elimu ya sekondari na elimu ya juu. Aidha, sera imeainisha vyombo mbalimbali vya ushauri katika ngazi pana zaidi kitaifa, kimkoa, kiwilaya na katika ngazi ya taasisi. Sera inaelekeza pia kuwa madaraka na uamuzi juu ya uongozi na utawala wa elimu kwenye ngazi ya wizara yatakasimiwa kwa vyombo vya chini yake na jamii.

Sera hii inasisitiza matumizi ya ukaguzi wa shule kama njia muhimu ya ufuatiliaji wa utoaji wa elimu na mafunzo kwa kuzingatia mtaala uliopo. Hali kadhalika huduma na ustawi wa walimu unazingatiwa kwa kupitia Idara ya Huduma kwa Walimu iliyo chini ya Tume ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

2.5 Elimu na Mafunzo Rasmi

Sera ya Elimu na Mafunzo inaeleza kuwa serikali inaruhusu na kutoa motisha kwa taasisi na watu binafsi kuanzisha na kuendeleza elimu na mafunzo rasmi nchini. Aidha, imeainisha lugha za kufundishia katika ngazi tofauti za elimu. Kwa elimu ya awali na msingi, Kiswahili kitumike kama lugha ya kufundishia na somo la lazima na hali kadhalika Kiingereza kuwa somo la lazima. Kwa elimu ya sekondari lugha ya kufundishia ni Kiingereza kwa ngazi zote na Kiswahili ni somo la lazima kwa sekondari ngazi ya kawaida.

Katika elimu na mafunzo rasmi, sera imefafanua kuwa uandikishaji na mahudhurio kwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule ni wa lazima kwa elimu ya msingi. Dhamira ya kuingiza kwenye mfumo rasmi elimu ya awali, kufanya elimu ya msingi kuwa ya wote na kuhimiza jamii kupanua utoaji wa elimu bora ya sekondari, imeleta uhitaji wa kuandaa walimu wengi zaidi. Hivyo, uanzishaji na umiliki wa vyuo binafsi vya ualimu

umeruhusiwa ili kukidhi mahitaji ya walimu wenye sifa kwa ngazi zote za elimu.

2.6 Mitaala, Mitihani na Utoaji Vyeti

Sera ya elimu na Mafunzo imeweka bayana kuwa mitaala ya shule huandaliwa na kuendelezwa ili kufikia malengo na madhumuni ya elimu ya jumla na maalum katika ngazi husika ya elimu. Taasisi ya Elimu Tanzania imepewa dhamana ya kuunda, kuendeleza, kufuatilia, kuhuisha na kuifanya iwe ya kisasa mitaala katika ngazi zote za elimu na mafunzo. Mtaala rasmi wa shule umelenga katika ufundishaji wa lugha, sayansi na teknolojia, masomo ya jamii, stadi za kazi na stadi za maisha ili kuweza kuendeleza utamaduni na kuhimili utandawazi. Mkazo kwenye maeneo hayo mapana utapenya kufikia ngazi zote za elimu na mafunzo.

Sera imefafanua kuwa mitihani itakuwapo kwa ajili ya kufuatilia, kutathmini na kuhimiza kufikiwa kwa malengo na madhumuni ya elimu na mafunzo yaliyowekwa na mitaala. Pia hutumika kupima maendeleo ya wanafunzi kwa kuzingatia ufaulu ili kuchaguliwa kwa tuzo ya cheti, kuendelea na elimu ya juu, na mafunzo ya kazi. Baraza la Mitihani la Tanzania limepewa dhamana ya kuwajibika kutunga, kudhibiti, kuendesha na kusimamia mitihani yote ya taifa. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania limekuwa ndicho chombo pekee kinachoruhusu, kuendesha na kusimamia mitihani yote ya nje ya nchi na hapa Tanzania.

Sera ya Elimu na Mafunzo imebainisha kuwapo kwa Bodi ya Huduma za Maktaba ambayo inahusika na kupanga, kuanzisha, kukuza, kutoa vifaa , kuongoza, kutunza na kuziendeleza maktaba za umma, shule na taasisi nyingine za elimu na mafunzo.

2.7 Elimu na Mafunzo ya Ufundi

Sera ya Elimu na Mafunzo inafafanua kuwa elimu na mafunzo ya ufundi stadi imewekwa ili kuwaandaa na kuwapa ujuzi wa kisasa watanzania kwa ajili ya kuajiriwa na kujiajiri kwenye shughuli mbalimbali za uchumi. Hivyo, pamoja na kujifunza stadi za kazi za kawaida, juhudi zinafanywa ili kuhakikisha kuwa watanzania wengi wanaendelezwa na kupata stadi halisi zinazohusiana na kazi. Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imepewa jukumu la kuandaa na kutoa maelezo, ushauri na mwongozo kuhusu elimu ya ufundi stadi. Vilevile imepewa dhamana ya kusajili na

kuthibitisha vituo vyote vya elimu na mafunzo ya ufundi. Aidha, wanafunzi kwenye mfumo rasmi wa shule watashauriwa juu ya manufaa na umuhimu wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Hali kadhalika, mafunzo ya stadi za biashara ni sehemu nyenza ya programu zote za elimu na mafunzo ya ufundi stadi.

Sera inafafanua kuwa mitihani yote na utoaji wa vyeti vya ufundi stadi utaratibiwa, kupangwa vizuri na kurekebishwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, na vyeti vitaonesha viwango vya maendeleo kwenye masomo yanayohusika.

Sera ya Elimu na Mafunzo inaeleza kuwa pamoja na Chuo cha Walimu wa Ufundi Morogoro, serikali ikishirikiana na asasi binafsi itaendelea kujenga na kuanzisha asasi zaidi za mafunzo ya walimu wa ufundi. Sera inatambua ukuzaji wa uwezo wa kiufundi kama moja ya vipaumbele vikubwa vya taifa. Kwa hiyo, kuna haja ya kuanzishwa kwa programu ya miaka 4 ya elimu ya ufundi baada ya elimu ya msingi kwenye mfumo wa shule. Kukiwa na upanuzi wa haraka wa elimu ya sekondari, idadi inayoongezeka ya wanafunzi wa kidato cha 4 na kidato cha 6 inaweza kujiunga na elimu ya mafunzo ya ufundi kwa kupitia vyuo vya ufundi mchanganyiko kwenye mfumo wa shule.

2.8 Elimu na Mafunzo ya Juu

Sera ya Elimu na Mafunzo imeainisha elimu ya juu kama ngazi ya tatu ya elimu baada ya elimu ya sekondari. Taasisi za elimu na mafunzo baada ya elimu ya sekondari na elimu ya juu hutoa mafunzo ya kitaalamu na hutuza vyeti, stashahada, shahada na stashahada za juu. Taasisi hizi zina utofauti wa hadhi za kisheria, miundo ya kiutawala na uendeshaji. Kutokana na ongezeko la mahitaji ya wataalamu wa ngazi za kati na juu na mahitaji ya kijamii ya elimu ya juu, uanzishwaji na umiliki binafsi wa taasisi za elimu na mafunzo baada ya elimu ya sekondari na elimu ya juu umeruhusiwa.

Taasisi za elimu na mafunzo baada ya elimu ya sekondari na elimu ya juu huandaa na kukuza mitaala yao ambayo huidhinishwa na Baraza la Mafunzo ya Ufundi na vyombo vingine vinavyohusika. Aidha, taasisi hizi zinaendesha na kusimamia mitihani na hutoa tuzo zinazostahili kama inavyotajwa kwenye sheria za taasisi hizo.

2.9 Elimu na Mafunzo Nje ya Mfumo Rasmi

Sera ya Elimu na Mafunzo inaeleza kuwa elimu na mafunzo nje ya mfumo rasmi wa elimu hugawanyika katika maeneo makubwa mawili: Elimu isiyo rasmi na Elimu ya Watu Wazima. Elimu isiyo rasmi inaelezwa kama mwenendo wa maisha yote ya kiutamaduni ambapo kila mmoja hupata mambo yenye maana kwake, ujuzi na maarifa kutokana na uzoefu wa kila siku na hali ya nyenzo zinazofanya ajifunze kwenye mazingira ya kiutamaduni na yale ya vitu vinavyomzunguka. Elimu ya watu wazima inaelezwa kuwa kimsingi inajishughulisha na uwezeshaji wa kujua kusoma, kuandika na kuhesabu na elimu ya kujiendeleza. Taasisi ya elimu ya watu Wazima imepewa jukumu la kuandaa, kukuza, kutoa na kufuatilia mtaala wa Elimu ya Watu Wazima na kisomo chenye manufaa. Programu nyingine za elimu ya kujiendeleza zitatumia mtaala unaoandaliwa na kukuzwa na taasisi husika. Kwa hiyo, taasisi zote za kielemu nchini zimetakiwa kuwa vituo vya Elimu ya Watu Wazima, na Wizara inayohusika na mafunzo ya ualimu itatoa mafunzo kwa kada maalum ya walimu na wakufunzi wa Elimu ya Watu Wazima.

2.10 Ugharimiaji wa Elimu na Mafunzo

Sera ya Elimu na Mafunzo imeeleza kuwa ugharimiaji wa elimu na mafunzo utachangiwa na serikali, jamii, wazazi na watumiaji wenyewe. Aidha, serikali hutoa motisha kwa watu binafsi, jamii na mashirika yasiyo ya kiserikali kuanzisha na kuendesha elimu na mafunzo kwa ngazi zote za elimu nchini. Karo na ada kwenye taasisi za serikali na binafsi zitapangwa kutokana na gharama halisi za elimu na mafunzo kwa kila ngazi. Kwenye taasisi binafsi, karo na ada zitapendekezwa na wamiliki na viongozi wa asasi hizo na kupewa kibali na serikali.

Sera imeeleza pia kuwa fungu la bajeti ya serikali linalotengwa kwa ajili ya elimu na mafunzo litaongezwa ili kuboresha huduma za elimu na mafunzo.

3.0 UTEKELEZAJI WA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO.

Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu na Mafunzo (ESDP) ya mwaka 1997, ilianzishwa kama hatua muhimu ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo. Mpango wa Maendeleo ya ELimu ya

Msingi (MMEM) 2002-2006 na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) 2004-2009, ni matokeo ya hatua hii muhimu.

3.1 Mafanikio ya Utekelezaji yaliyotokana na Mpango wa Elimu MMEM na MMES.

3.1.1. MMEM.

- Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji, zimeagizwa kufungua madarasa ya elimu ya awali katika shule za Msingi za serikali nchini. Aidha wadau wengine pia wanahamasishwa na kuhimizwa kuwekeza katika elimu ya awali nchini kote.

- Wanafunzi wa shule za Msingi wameongezeka kutoka millioni 3.8 mwaka 1995 hadi millioni 7.5 mwaka 2005.

- Shule za Msingi zimeongezeka kutoka 10, 927 mwaka 1995 hadi 14, 257 mwaka 2005.

- Kuanzia mwaka 2002-2005 yamejengwa madarasa 45,000, nyumba za walimu 8, 527, matundu ya vyoo 98,827 na kununuliwa madawati 285,898.

3.1.2 MMES.

- Wanafunzi wanaojiunga kidato cha 1 wameongezeka kutoka 53, 698 mwaka 1995 hadi 180, 239 mwaka 2005.

- Wanafunzi wa Kidato cha 1- 4 wameongezeka kutoka 183,659 mwaka 1995 hadi 489,942 mwaka 2005 wakiwemo wasichana 231,808.

- Wanafunzi wanaojiunga na Kidato cha 5 wameongezeka kutoka 6,875 mwaka 1995 hadi 18,893 mwaka 2005.

- Wanafunzi wa Kidato cha 5-6 wameongezeka kutoka 12,716 mwaka 1995 hadi 34, 383 mwaka 2005, wakiwemo wasichana 12,763. Kwa hiyo jumla ya wanafunzi wa Kidato cha 1-6 imeongezeka kutoka 196,375 mwaka 1995 hadi 524, 325 mwaka 2005 wakiwemo wasichana 244, 551.

- Shule za Sekondari zimeongezeka kutoka 595 mwaka 1995 hadi 1,755 mwaka 2005 zikiwemo 543 zisizo za serikali.

3.1.3 ELIMU YA UALIMU.

- Idadi ya walimu tarajali katika vyuo vya Ualimu imeongezeka kutoka 12, 417 mwaka 1995 hadi 29,952 mwaka 2004.

- Idadi ya vyuo vya Ualimu vya serikali na visivyo vya serikali imeongezeka kutoka 34 mwaka 1995 hadi 52 mwaka 2005.

- Ili kuongeza idadi ya walimu wenye shahada na stashahada ya elimu, kuanzia mwaka 2005 shule za sekondari za Mkwawa na Chuo cha Ualimu Dar-es-Salaam, vimebadilishwa kuwa vyuo vikuu vishiriki vya elimu ya chuo kikuu cha Dar-es-Salaam, na chuo cha Ualimu cha Mtwara kimekuwa chuo ambata cha Elimu cha chuo kikuu cha Dar-es-Salaam.

- Mafunzo ya Kompyuta na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano yameanzishwa katika vyuo vyote vya ualimu na kufanywa kuwa masomo ya lazima kwa kila mwalimu tarajali.

- Kuhakikisha kuwa mapengo ya walimu katika shule za Msingi na Sekondari yanazibwa:

    - Walimu wapya 45,451 wakiwemo 37, 261 wa daraja A, 7, 152 wa stashahada waliajiriwa kati ya mwaka 2000 na 2005.

    - Kuanzia mwaka 2003 wanafunzi wa mafunzo ya ualimu tarajali wamekuwa wakiajiriwa moja kwa moja baada ya kuhitimu mafunzo.

    - Kati ya mwaka 2000 na 2005 vibali vya ajira mbadala viliombwa na kutolewa ili kujaza mapengo ya jumla ya walimu 1,134 walioacha kazi kwa sababu mbalimbali.

3.1.4 ELIMU NJE YA MFUMO RASMI

- Ili kupunguza ongezeko la watoto na vijana wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu, mpango wa Elimu ya Msingi kwa watoto walioikosa (MEMKWA) umeanzishwa katika makundi rika mawili, miaka 11-13 na 14-18 kwa elimu nje ya shule kwa mfumo usio rasmi.

- Katika kuhusiana, Elimu ya watu Wazima na Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA) umetolewa kwa kutumia mbinu shirikishi.

3.1.5 UGHARIMIAJI WA ELIMU.

- Katika kugharimia elimu na mafunzo nchini, bajeti ya elimu imeongezeka kutokana na mikopo ya masharti nafuu kutoka vyombo vya kifedha vya dunia, hususan Benki ya Dunia. Pia misaada ya wahisani imeweza kupatikana kwa ajili ya MMEM na MMES.

- Bajeti ya elimu imeongezwa kutoka asilimia 21.8 mwaka 1999/2000 hadi kufikia asilimia 37.3 mwaka 2004/05. Pamoja na ongezeko hilo, bado Bajeti haikidhi malengo.

- Ushirikiano na wadau wa elimu umeimarishwa kupitia vikao vya pamoja vya kamati ya uongozi wa Maendeleo ya Elimu (ESDP - Inter-Ministerial Steering Committee), Kamati ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (Basic Education Development Committee), na vikundi vya Kamati za kiufundi (Technical Working Groups).

3.1.6 Uhuishaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo.

Sera ya Elimu na Mafunzo 1995, ina miaka takriban kumi sasa tangu ianze kutumika. Sera hiyo imeweka wazi madhumuni na malengo ya elimu na mafunzo na miongozo ya jumla ya utekelezaji wake kwa nyanja zote za elimu.

- Madhumuni, malengo na matarajio ya Sera ya Elimu na Mafunzo yanashabihiana na yale ya Dira ya Taifa ya mwaka 2025 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini pamoja na Mtazamo wa Jumla wa kiserikali (Sector-wide Approach) unaosisitizwa na programu ya kuboresha sekta ya elimu na mafunzo.

- Hivi sasa sera ya Elimu na Mafunzo inaangaliwa upya kwa kuzingatia mabadiliko mbalimbali yaliyojitokeza na matarajio ya siku zijazo, hivyo kubaini mapengo yaliyomo pamoja na kupata maoni ya wadau mbalimbali wa elimu kuhusiana na mabadiliko ya Sera hiyo.

4.0 CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI

- Ukosefu wa usahihi katika kutafsiri miongozo na maelekezo ya programu za MMEM na MMES ambao umesababisha baadhi ya

wadau, wasimamizi na watendaji wasiweze kutekeleza majukumu yanayotakiwa na programu hizi.

- MMES imekuwa na tatizo la kuwa na pengo kubwa la kifedha kutokana na kuwa na chanzo kimoja tu cha fedha ambacho ni mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia.

- Kuwapo kwa tatizo la uelewa mdogo juu ya uendelevu wa programu ya MMEM kwa baadhi ya wadau na watendaji wakidhani kuwa utekelezaji wa programu hii mwisho wake ni mwaka 2006 na hivyo kupunguza juhudi za kusimamia utekelezaji wake.

- Kuwapo kwa tatizo la kuchelewa kuziba pengo la MMEM kutokana na kumalizika kwa mkataba wa miaka mitatu wa kupata fedha kutoka Benki ya Dunia.

5.0 MAAMUZI MUHIMU KWA UTEKELEZAJI WA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO

- Kuimarisha MMEM kwa kuandaa Awamu ya Pili ya MMEM 2007 - 2015 kwa madhumuni ya kuwa na mpango endelevu ili kufikia malengo ya EFA na MDGs.

- Kuimarisha utekelezaji wa programu ya MMES 2004 -2009 kwa kuzijengea shule za sekondari uwezo wa kupokea, kutunza na kutumia fedha za ruzuku ya uendeshaji na ruzuku ya maendeleo kwenye akaunti zao za shule.

- Kuendelea kuimarisha mitaala ya elimu ya sekondari ili kukidhi haja ya mabadiliko yanayoendelea ya utandawazi, ushindani wa kiuchumi na uboreshaji wa elimu.

- Kuimarisha ufuatiliaji, tathmini na uwezeshaji wa MMEM na MMES ili kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa.

- Uanzishwaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundi (Vocational Education Development Plan - VEDP) kwa ajili ya kupanua mafunzo ya ufundi kwa ajili ya wanafunzi ambao hawataendelea ngazi inayofuata ya elimu ya kawaida kwa ajili ya kukuza ajira kulingana na mahitaji ya soko.

- Uanzishwaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu (Higher Education Development Plan) ili kumudu ongezeko kubwa la wahitimu wa Kidato cha 6.

- Maandalizi ya awamu ya pili ya MMES kwa lengo la kufikia Elimu ya Sekondari kwa Wote (Universal Secondary Education) ifikapo mwaka 2015.

- Kuchambua na kuhuisha Sera ya Elimu na Mafunzo ili kukabiliana na mabadiliko ya utandawazi na ushindani unaoendelea duniani kote.

- Kushusha madaraka ya Elimu ya Sekondari karibu na walengwa